

Maswali elekezi ya kurekebisha na kuboresha mkakati wa upanuzi

Baada ya mkakati wa awali wa upanuzi kuundwa, unaweza kushawishika kufikiria kuwa “umekamilika” na kuelekeza umakini na nguvu katika utekelezaji wa mkakati huo. Hata hivyo, upanuzi ni mchakato unaorudiwarudiwa unaohitaji marekebisho endelevu, uboreshaji na usahihihaji wa mwelekeo kulingana na data iliyokusanywa, mafundisho yaliyopatikana, na mabadiliko katika mazingira mapana ya elimu, kama vile sera mpya au mabadiliko ya uongozi.

Maswali haya elekezi yameundwa ili kujalizia uundaji wa mkakati wa kuongeza na kupanua matokeo ya mpango wa elimu au uvumbuzi.¹ Yanakusudiwa kuwasaidia watu na taasisi zinazoendelea na mchakato wa upanuzi kutafakari mara kwa mara na kwa ushirikiano kuhusu matatizo na fursa zinazojitokeza zinazohusiana na mkakati wa upanuzi, ili KUPANGA na KUJARIBU marekebisho, na KUFIKIRIA na KUREKEBISHA mabadiliko haya mara kwa mara. Lengo kuu ni kuwezesha na kuimarisha mchakato wa kupanua athari katika elimu.

Hatua Ya 1: Panga

Jikumbushe: Je, lengo kuu la upanuzi ni lipi?

Lengo la upanuzi linapaswa kuwa maalum, linalopimika na lenye muda maalum wa kutekelezwa. Lengo hili linapaswa kutoka moja kwa moja kwenye mkakati wa upanuzi ambao tayari umeunda.

Tambua tatizo au fursa

- Je, kuna tatizo au changamoto kuu inayotokea katika mchakato wa upanuzi unayotaka kushughulikia au fursa mpya unayotaka kutumia?
- Ni kwa nini tatizo au fursa inatokea? Jaribuni kujiuliza “ni kwa nini?” mara kadhaa ili kufanya uchanganuzi wa kina na kuelewa chanzo cha msingi cha tatizo au fursa.²

1. Ikiwa bado hujaweka lengo wazi la upanuzi pamoja na mkakati wa kulifikia, tunapendekeza uanze kwa kupitia makala ya “Miongozo ya mkakati wa upanuzi,” ambayo inatoa mwongozo wa kufafanua lengo wazi la upanuzi, linalopimika na lenye muda maalum wa kutekelezwa, pamoja na mkakati wa kiwango cha juu unaotumika kama “nyota ya kaskazini” ya kuongoza juhudi za upanuzi na pia kama hati ya mipango inayobadilishika ambayo inaweza kurejelewa na kusasishwa mara kwa mara kulingana na maarifa mapya, data na mabadiliko ya mazingira.

2. Taasisi ya Lean Enterprise imeunda video muhimu ya ufafanuzi ya mbinu hii rahisi ya kutambua vyanzo vya msingi vya matatizo (na rasilimali nyingine nyingi zipo mtandaoni): <https://youtu.be/SrYkx41wEE>



Tafakari

Je, kuna marekebisho, mabadiliko au uboreshaji unaoweza kufanya ili kushughulikia tatizo hili au kutumia fursa hii?



Panga jinsi utakavyotekeleza na kufanyia majaribio mabadiliko au marekebisho haya

- Je, ni kazi gani kuu zinazohusika katika kutekeleza marekebisho haya?
- Je, majaribio yatafanywa lini? Kwa muda gani?
- Je, jaribio litafanyika wapi? Katika vituo vingapi?
- Je, kuna mambo ya kuzingatia kuhusu mazingira? Matatizo ya usawa?



Zingatia vipimo na gharama

- Je, utatathmini vipi iwapo marekebisho haya yanafaa? Je, unatumai marekebisho yatasababisha mabadiliko gani? Je, utahitaji data gani? Je, ni nani atakusanya na kuchanganua data hiyo? Mara ngapi?
- Ni rasilimali gani zitahitajika na zitatoka wapi?
- Inaweza kuwa vigumu kuona mabadiliko ya haraka au maendeleo katika mikakati ya muda mrefu. Je, kuna viashiria vya mapema unavyoweza kutafuta ili kuona kama marekebisho yana athari (chanya au hasi)?

Hatua Ya 2: Fanya Majaribio Na Kupima

Mara nyingi, kila marekebisho au uboreshaji wa mkakati wa upanuzi utapitia mizunguko mingi ya majaribio na mabadiliko. Hakuna muda maalum wa kudumu kwa mizunguko hii na utategemea marekebisho yaliyojaribiwa, vipimo vilivyokusanywa na hatua ya mchakato. Kwa mfano, majaribio ya mapema ya wazo yanaweza kuwa ya haraka kuliko marekebisho ya baadaye. Hata hivyo, ni muhimu kwamba mizunguko iwe mifupi vya kutosha ili data iliyokusanywa iendelee kuwa inayofaa kwa wakati husika, inayosaidia na muhimu ili kutoa mafundisho ya haraka na kufanya maamuzi.



Bainisha muda

- Kwa mzunguko huu, unatazamia kuona athari au mabadiliko yoyote lini?
- Mzunguko huu wa majaribio unapaswa kuisha lini?

Hatua Ya 3: Waza Na Kusahihisha

Waza kuhusu kilichotokea

- Jikumbushe lengo la upanuzi na kwa nini unayapa marekebisho haya kipaumbele.
- Matokeo ya majaribio ya marekebisho hayo ni yapi? Ni nini kilikuwa na ufanisi na ni nini hakikuwa na ufanisi?
- Je, kulikuwa na marekebisho yoyote ya ghafla au ambayo hayakupangwa yaliyofanywa kwenye mpango wa awali?
- Je, matokeo yalikuwaje yakilinganishwa na ubashiri? Je, kulikuwa na matokeo yoyote ambayo hayakutarajiwa?

Panga kinachofuata

Utafanya nini kulingana na fundisho na wazo hili? Je, unapanga kuingiza marekebisho haya kikamilifu katika mkakati wako wa upanuzi? Je, unahitaji kuendelea kufanyia marekebisho haya majaribio? Unataka kuachana nayo ili ujaribu kitu kingine? Bila kujali hatua yako inayofuata, tambua mafundisho machache muhimu uliyojifunza kuhusu mchakato huu yanayoweza kuelekeza mbinu yako ya kuu ya upanuzi.

Hatua Ya 4: Anza Tena

2026

Zana hii ilitengenezwa na Jenny Perlman Robinson, Molly Curtiss Wyss na Patrick Hannahan, pamoja na michango kutoka kwa washirika wetu wengi wa Real-time Scaling Lab, wanachama wa Kikundi cha Ushauri, wanagenzi na wafanyakazi wenza wengine. Pia tunatoa shukrani zetu kwa Katie Portnoy na Esther Rosen kwa usaidizi wao wa uhariri na usanifu. Ili kushiriki uzofu wako wa kutumia zana hii au kutoa maoni yoyote kwa ajili ya matoleo yajayo, tafadhali tuma barua pepe kwa CUR@brookings.edu.

Zana hii ni sehemu ya mfululizo kuhusu upanuzi unaowezeshwa na usaidizi kutoka kwa Wakfu wa Bernard van Leer, Wakfu wa BHP, ELMA Philanthropies, Inc. kupitia Kampeni ya Elimu ya Wanawake (CAMFED), Kituo cha Utafiti wa Maendeleo ya Kimataifa, Kanada kupitia Wakfu wa Elimu na Maendeleo ya Teknolojia ya Habari (FIT-ED), Kamati ya Uokoaji ya Kimataifa na Wakfu wa Jacobs. Maoni yaliyotolewa katika zana hii ni ya waandishi wake na hayawakilishi maoni ya wafadhili, maafisa wao, wafanyakazi au Bodi za Magavana.